

# Mtaalamu tiba ya saratani kuwasili

## DAR ES SALAAM

MTAALAMU bingwa wa maradhi mbalimbali ya saratani kutoka India, Dkt. Ps Sridhar anatarajiwa kuwasili nchini leo kwa ajili ya kuwafanyia uchunguzi wagonjwa wenye maradhi hayo, **anaripoti Mwandishi Wetu.**

Mwenyekiti wa Hospitali ya Regency itakapofanyika kliniki hiyo, Dkt. Rajni Kanabar, alisema kuwa kliniki hiyo itafanyika Jumapili kwenye hospitali hiyo jijini Dar es Salaam.

Alisema mtaalamu huyo anatoka hospitali kubwa ya saratani ya Asia Kusini ya HCG Group, Bangalore, India.

Alisema hiyo ni fursa muhimu kwa Watanzania wenye matatizo hayo kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa afya zao na

kupatiwa ushauri wa namna ya kupata tiba.

"Hii ni fursa nyeti sana kwa wagonjwa wote wa saratani na wale waliokwisha pata tiba India, wanaweza kuja kuangaliwa maendeleo yao hali ambayo itaokoa fedha za kwenda India kwa kuangalia maendeleo ya afya zao," alisema.

"Mtaalamu ataangalia kama wanahitaji matibabu zaidi ama wanahitaji tiba ya aiba gani, watu waje wamwone mtaalamu kwa ajili ya uchunguzi zaidi na ushauri wa kitaalamu," alisema Dkt. Kanabar.

Alisema hospitali hiyo ya India imeanzisha ushirikiano na Regency kwa ajili ya kusaidia Watanzania wanaolazimika kwenda India kwa matibabu kuweza kuokoa fedha zao.

MAJIRA 09.DEC.2011